# MISINGI YA KIBIBLIA: Mwongozo wa Kozi

**Ufalme, Maagano & Kanoni ya Agano la Kale**
**Ufalme na Agano katika Agano Jipya**

## MAELEZO YA KOZI

Kozi hii inawasilisha kwa ufupi dhamira kuu mbili za kibiblia kwa kuchunguza ufalme wa Mungu na utekelezaji wa maagano ya ki-ungu, pamoja na somo moja linalohusu mfumo wa kuundwa kwa kanoni ya Biblia. Katika kozi hii tutaona kwamba, Agano la Kale na Agano Jipya siyo tu mkusanyiko na mchanganyiko wa hadithi mbalimbali, au mafundisho na habari za kinabii. Badala yake, yote yameungana katika dhamira kuu ya ufalme wa Mungu, ambayo imewasilishwa kupitia maagano. Kozi hii imejengwa katika mfululizo wa video mbili za Thirdmill, ***Ufalme, Maagano & Kanoni ya Agano la Kale***, **na** ***Ufalme na Maagano katika Agano Jipya.*** Kozi na video hizo zimeandaliwa na Third Millennium Ministries na kuwasilishwa na Dk. Richard L. Pratt, Jr. pamoja na Dk. Simon Vibert.

## MALENGO YA KOZI, MAKUSUDI NA ORODHA YA MODULI

### *Malengo*

Katika kozi hii, tunapenda kufikia malengo yafuatayo:

1. Tunatarajia kuwa, utatumia vipengele vyote vya kozi hii ili uweze:
    - Kuelewa umoja wa Agano la Kale na Agano Jipya, kama ilivyoelezwa katika dhamira ya Ufalme wa Mungu;
    - Kulielewa kusudi la Mungu katika historia ya Agano la Kale na Agano Jipya, kama inavyoelezwa katika maagano; na
    - Kugundua namna mafundisho yake yanavyopaswa kutumika katika maisha yetu ya sasa.
2. Tunatarajia kuwa, utapata shauku kubwa ya kujifunza Agano la Kale na Agano Jipya.
3. Tunatarajia kuwa, maisha yako yatabadilika kutokana na mafundisho ya kozi hii. Na kuwa itakusaidia kuelewa na kutumia vifungu mbalimbali vya Maandkio ya Biblia nzima.

### *Makusudi*

Kwa kufanya mambo yafutato, itakuwa ishara kuwa malengo haya yamefikiwa:

1. Kupata alama za kuridhisha katika mitihani na majaribio, na kwamba unaweza kubaini:
    - Dhana kuu ya Ufalme wa Mungu, kama inavyoelezwa Agano la Kale na Agano Jipya;
    - Maagano muhimu ya Agano la Kale na kueleza mahusiano yake na Agano Jipya; n
    - Kubaini kanuni sahihi za namna ya kutumia Agano la Kale na Agano Jipya kwa sasa.
2. Kukamilisha miongozo yote ya somo na kazi zingine zote za darasani kwa kozi husika. Kuelezea mawazo na mitazamo yako juu ya Agano la Kale na kuonesha namna ulivyotumia mafundisho hayo katika maisha yako mwenyewe. Hasa kwa kuzihirisha

kwamba umezingatia umoja wa Agano la Kale, historia ya maagano, na dhamira ya ufalme wa Mungu katika kufafanua na kutumia vifungu vya Agano la Kale.

3. Kushiriki katika mijadala ya kila wiki ambayo inakufanya kupitia na kutafakari mafundisho yatokanayo na video za Thirdmill, ili kufahamu zaidi mawazo muhimu na kuyatumia katika maisha yako na huduma yako.

**Orodha ya Moduli kwa Kozi ya Misingi ya Kibiblia**

1. Kwa nini Tusome Agano la Kale?
2. Ufalme wa Mungu katika Agano la Kale
3. Maagano ya Ki-Mungu
4. Kanoni ya Agano la Kale
5. Kwanini Tujifunze Agano Jipya?
6. Ufalme wa Mungu katika Agano Jipya
7. Agano Jipya

## MAELEZO KUHUSU VIPENGELE VYA KOZI

**Beji**

1. Kila juma katika mazungumzo yenu mtatenga muda kwaajili ya kufanyia kazi vipengele vya Beji. Mwongozo huu wenye kurasa mbili utampa mkufunzi wenu mwongozo wa jumla wa namna mnavyotakiwa kuendeleza ujuzi huu muhimu katika huduma.
2. Katika wiki chache za mwanzoni, tumia muda wako ukiwa na kikundi chako pamoja na mkufunzi wako kupitia mada za kujadili kwenye maelezo ya beji.
3. Baada ya kuweka msingi imara kupitia majadiliano ya kikundi, tumia wiki zilizobaki kuifanyia kazi beji (mambo ya kufanya).
4. Utapatiwa beji pale mkufunzi wako atakapojiridhisha kuwa umetimiza vigezo vya beji kwa mujibu wa maelekezo yake.

**Moduli**

1. Jifunze kwa kutazama video, kusikiliza sauti, au kusoma nukuu.
2. Kamilisha mwongozo wa kujifunza kwa kila somo. Miongozo ya kujifunza itakuandaa wewe kujibu maswali ya mitihani, mazoezi ya kwenye mitandao na kukusaidia kuyatumia mafundisho ya somo katika maisha yako binafsi.
3. Fanya mitihani ya kila somo, mitihani itatolewa na mkufunzi wako. Mitihani inaweza kurudiwa kama kuna ulazima, tunapendekeza ufikie alama zaidi ya asilimia 80% kabla ya kushiriki mjadala wa wiki na kuhakikisha kuwa umeelewa maneno kwa usahihi.
4. Shiriki katika majadiliano ya kila wiki kwenye kundi lako pamoja na mkufunzi wako, mkitumia miongozo kuhusu kozi na uwezo wa kutumia maneno kwa usahihi katika maisha yako au huduma yako. Tunapendekeza mijadala kupitia video isiwe chini ya saa limoja.

**Mtihani wa Mwisho**

Unaweza ukafanya majaribio zaidi ya mara moja kama ukihitaji kujipima, lakini unatakiwa ujifunze na kusubiri kwa muda wa saa moja kabla ya kufanya jaribio jingine. Alama yako rasmi itakuwa ile uliyofanya vizuri zaidi kwenye majaribio yako na tunapendekeza upate zaidi ya 80% kabla ya kuendelea na kozi inayofuata.

**Alama za Ufaulu**

Daraja la mwisho la ufaulu litahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Majaribio ya darasani yatakuwa na alama 30 kila moja.
2. Mtihani wa mwisho utakuwa na alama 100.
3. Ripoti ya beji ya maombi haiwezi kubadilisha daraja lako lakini ni lazima ipitishwe na mkufunzi ili uwe umekamilisha kozi.

*Alama za jumla katika kozi zinazozidi 80% zinahesabiwa kuwa ni ufaulu.*

---

**Walioshiriki Kuandaa kozi hii**

- **Dk.David R, Bauer** ni Mkuu wa kitivo cha kutafsiri Biblia na cha Ralph Waldo Beason Profesa wa Chuo cha ufafanuzi katika Seminari ya Thiolojia ya Asbury.
- **Dk. Rick Boyd** ni Profesa wa Ufafanuzi wa Kibiblia katika seminari ya Wesley Biblical Seminary.
- **Dk. Constantine R. Campbell** ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School.
- **Dk. D.A. Carson** ni Profesa wa Utafiti wa Agano Jipya katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School na mwasisi mwenza wa The Gospel Coalition.
- **Dk. Robert B. Chisholm, Jr.** ni mwenyekiti wa kitengo na Profesa wa Agano la Kale katika seminari ya Dallas Theological Seminary.
- **Dk. Ashish Chrispal** ni Mkurugenzi wa Kanda ya Asia Asia kwa ajili ya Baraza la Nje.
- **Dk. David Correa** ni Profesa Mshiriki katika seminari ya San Pablo Theological Seminary huko Merida, Mexico na Mkurugenzi wa Next Institute Mexico. Pia anatumika kama mchungaji wa kanisa la Presbyterian Iglesia Jesus huko Progreso.
- **Dk. Brandon D. Crowe** ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika seminari ya Westminster Theological Seminary.
- **Mwl. Sherif Atef Fahim** mwalimu wa thiolojia katika chuo cha Alexandria School of Theology huko Misri.

- **Mch. Michael J. Glodo** ni Profesa Mshiriki wa Masomo ya Biblia katika chuo cha Reformed Theological Seminary huko Orlando, Florida.
- **Dk. Douglas Gropp** aliwahi kuwa Profesa wa Agano la Kale na Mwalimu wa Taaluma katika seminari ya Redeemer Seminary.
- **Dk. James M. Hamilton** ni Profesa mshiriki wa Thiolojia ya Kibiblia katika seminari ya Southern Baptist Theological Seminary na mchungaji wa kanisa la Kenwood Baptist Church.
- **Dk. Joel C. Hunter** ni mchungaji kiongozi wa kanisa la Northland, Kanisa lililoenea huko Longwood, FL.
- **Mch. Clete Hux** ni Mkurugenzi na Mtetezi dhidi madhehebu yasiyo ya Kikristo huko Birmingham, AL.
- **Dk. Thaddeus J. James, Jr.** ni makamu wa raisi wa mambo ya taaluma katika seminari ya Birmingham Theological Seminary.
- **Dk. Mark A. Jennings** Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Bw. Bradley T. Johnson** ni Profesa Mshiriki katika seminari ya Asbury Theological Seminary na mchungaji wa kanisa la Wesley Chapel UMC in Nicholasville, KY.
- **Dk. Dennis E. Johnson** ni Profesa wa Thiolojia kwa Vitendo katika seminari ya Westminster Seminary California.
- **Dk. Jim Jordan** ni mkufunzi wa kimataifa katika taasisi ya Training Leaders International.
- **Dk. Edward M. Keazirian** ni Profesa Msaidizi wa lugha ya Kiyunani na Mkurugenzi wa Lugha ya Kiyunani katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Craig Keener** Mkuu wa kitivo cha Masomo ya Biblia katika seminari ya Asbury Theological Seminary.
- **Dk. Daniel Kim** hufundisha Agano la Kale katika seminari ya Covenant Theological Seminary.
- **Mch. Kevin Labby** ni mchungaji kiongozi katika kanisa la Willow Creek Church huko Winter Springs, FL.
- **Dk. Dan Lacich** hutumika katika timu ya wachungaji katika kanisa la Northland, A Church Distributed, in Orlando, FL.

- **Dk. Richard Lints** ni Profesa wa Thiolojia na makamu wa raisi kwa ustawi wa kitaaluma katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Robert MacEwen** ni mhadhiri wa masomo ya Kibiblia na Mkurugenzi wa kitengo Chinese Theology Department katika chuo cha East Asia School of Theology, Singapore.
- **Dk. Sean McDonough** ni Profesa wa Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Mch. Timothy Mountfort** ni mwalimu wa taaluma katika seminari ya Western China Covenant Theological Seminary.
- **Dk. Matthew Newkirk** ni Mkuu wa Chuo na Profesa wa Agano la Kale katika seminari ya Christ Bible Seminary in Okazaki, Japan.
- **Dk. Jeffrey J. Niehaus** ni Profesa wa Agano la Kale katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Jason Oakes** ni Profesa Mshiriki wa Mawazo wa Kikristo katika chuo cha Talbot School of Theology.
- **Dk. Luis Orteza** ni Profesa Msaidizi wa Ushauri katika seminari ya Birmingham Theological Seminary.
- **Dk. Grant R. Osborne** (1942-2018) alikuwa Profesa wa Agano Jipya katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School.
- **Dk. John Oswalt** ni Profesa wa masafa wa Agano la Kale katika seminari ya Asbury Theological Seminary.
- **Dk. Alvin Padilla** ni mlezi wahuduma iitwayo Hispanic Ministries na Profesa wa Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Jonathan T. Pennington** ni Profesa Mshiriki wa Ufafanuzi wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa Utafiti wa Masomo ya Kizamivu katika seminari ya The Southern Baptist Theological Seminary.
- **Dk. Gregory R. Perry** ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa huduma iitwayo City Ministry Initiative katika seminari ya Covenant Theological Seminary, St. Louis, MO.
- **Yohanes Praptowarso, Ph.D.** hutumika katika seminari ya Batu Theological Seminary.
- **Dk. Clay Quarterman** alikuwa rais wa chuo cha Evangelical Reformed Seminary huko Ukraine mpaka alipostaafu mwaka wa 2019.

- **Dk. Scott Redd** ni Mkuu wa kambi ya seminari ya Theological Seminary huko Washington D.C. na Profesa Mshiriki wa Agano la Kale.
- **Mch. Ric Rodeheaver** ni mchungaji kiongozi wa kanisa la Christ Community Church huko Laguna Hills katika jimbo la California.
- **Dk. Mike Ross** hufundisha Thiolojia kwa Vitendo katika seminari ya Reformed Theological Seminary, Charlotte, NC, na hapo awali alikuwa mchungaji kiongozi wa kanisa la Christ Covenant Church huko Matthews, NC.
- **Dk. Brian D. Russell** ni Profesa wa Masomo ya Kibiblia na Mlezi wa shule kwa huduma za mjini katika seminari ya Asbury Theological Seminary in Orlando, FL.
- **Dk. Philip Ryken** ni raisi wa chuo cha Wheaton College.
- **Dk. Eckhard Schnabel** ni Profesa wa Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Glen Scorgie** ni Profesa wa Thiolojia katika seminari ya Bethel Seminary's San Diego Campus.
- **Dk. Daniel Simango** ni mkuu wa chuo cha The Bible Institute of South Africa huko Cape Town.
- **Dk. Vuyani Sindo** ni mhadhiri katika chuo cha George Whitefield College huko Africa Kusini.
- **Dk. Daniel Steffen** ni Profesa wa masafa katika seminari ya Seminario Teológical Centroamericano huko Guatemala City.
- **Dk. Mark L. Strauss** ni Profesa wa Agano Jipya katika seminari ya Bethel Seminary, San Diego.
- **Dk. Derek Thomas** ni Profesa wa Thiolojia ya Kimfumo na Kihistoria katika seminari ya Reformed Theological Seminary huko Atlanta, GA.
- **Mch. Dr. Simon Vibert** aliwahi kuwa kiongozi wa kanisa la St. Luke’s Church, Wimbledon Park, UK, na kwa sasa ni makamu mkuu wa chuo cha Wycliffe Hall, Oxford, na mkurugenzi wa Shule ya mahubiri.
- **Dk. Peter Walker** ametumika kama Profesa wa Masomo ya Kibiblia katika chuo cha Trinity School for Ministry na makamu mkuu wa chuo mshiriki wa chuo cha Wycliffe Hall, Oxford. Kwa sasa ni mshauri mwelekezaji wa kituo cha Jerusalem Center kwa Masomo ya Kibiblia.

- **Dk. Stephen J. Wellum** ni Profesa wa Thiolojia ya Kikristo katika seminari ya The Southern Baptist Theological Seminary.
- **Dk. Stephen E. Witmer** ni Profesa Msaidizi wa Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.
- **Dk. Jonathan D. Worthington** ni mkurugenzi wa kuandaa mitaala katika taasisi ya Training Leaders International.